JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

LATRA

# UFAHAMU MFUMO WA TAARIFA KWA ABIRIA PIS




*pis.latra.go.tz*


***Pamoja kwa Usafiri Bora***

# UFAHAMU MFUMO WA TAARIFA KWA ABIRIA (PIS)

Ni ukweli usiopingika kwamba, abiria wengi wamekuwa wakikumbana na kadhia mbalimbali za usafiri pindi watumiapo usafiri wa umma ikiwemo usafiri wa mabasi ya masafa marefu au kama ilivyozoeleka kama mabasi yanayoenda mikoani.

Msomaji wa makala hii, nikurudishe kidogo miaka ya nyuma, kumbuka namna ulivyokuwa ukitumia muda mwingi kumsubiri ndugu/ jamaa/rafiki yako aliyetoka mkoa mmoja kwenda mkoa uliopo, tafakari muda ulioupoteza kipindi unamsubiri ndugu yako ambaye hukufahamu atawasili muda gani kwenye kituo cha mabasi ulichokuwepo, fikiria ulivyokuwa ukisubiri gari unalosafiri kwenda mkoa mwingine bila kufahamu muda halisi wa basi hilo kufika, tafakari ulivyokuwa ndani ya basi na kuona jinsi basi ulilopanda lilivyokuwa likienda kwa kasi isiyo ya kawaida na pia fikiria zile ajali ambazo zilitokana na ukosefu wa upatikanaji wa taarifa za mwendo wa basi kwa abiria. Bila shaka kwa kipindi kile ulikuwa unajiuliza, hivi hali hii mpaka lini?!

Changamoto hizo pia ziliinyima usingizi Serikali hasa kwa kuwa maisha ya watanzania wengi wasio na hatia yalipotea ikiwemo kupoteza nguvu kazi ya Taifa. Jambo hili liliifanya Serikali kutafuta suluhu ili kupunguza kadhia hizo ambapo kutokana na uwepo wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na




| NA. | MMILIKI (OWNER) | NAMBA YA GARI (REG NO) | KUTOKA (FROM) | KWENDA (TO) | KUFIKA (ARRIVALS) | MUDA (TIME) | TAARIFA YA MWISHO (LAST LOCATION) | MUDA WA TAARIFA YA MWISHO (TIME) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 13 | MUSSA HEMED BASUKA (TAWASAL) | T309DPJ | DAR ES SALAAM | DODOMA | 2024-09-03 | 11:49 Jioni | 0.49 KM NE OF BUNGE | N/A |
| 14 | SUPER BARAKA FAMILY | T311DCN | DAR ES SALAAM | DODOMA | 2024-09-03 | 2:27 Usiku | 0.19 KM N OF ROUND ABOUT AIRPORT | 11:18 Jioni |
| 15 | ISAMILO EXPRESS | T312EHD | MWANZA | DAR ES SALAAM | 2024-09-04 | 3:47 Asubuhi | 4.35 KM NW OF MASWA-BARIADI JUNCTION | 11:46 Jioni |

Mawasiliano (TEHAMA), mifumo mbalimbali ya TEHAMA imebuniwa na kuanza kutumika katika sekta ya usafiri ardhini nchini.


Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inahusika moja kwa moja na kuboresha sekta hii na inatumia mifumo ya TEHAMA inayosaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto hizo. Miongoni mwa mifumo madhubuti na thabiti uliobuniwa na unaotumiwa na wadau wa sekta ya usafiri ardhini hususan wanaosafiri na mabasi ya masafa marefu ni Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwenye simu janja kupitia kivinjari (browser) chochote kwa anwani ya https://pis.latra.go.tz uliozinduliwa rasmi mwezi Julai mwaka 2024.

Akiuzungumzia mfumo wa PIS, Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi anawapongeza LATRA kwa kubuni Mfumo huo ambao ni sehemu ya mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na amesema PIS imekuja wakati muafaka ambapo Serikali inafanya kila iwezalo kupunguza ajali nchini na anaamini

kupunguza ajali nchini na anaamini mfumo huo unaenda kutekeleza hilo.

Aidha, Mhe. Kihenzile anaeleza kuwa takwimu za ajali ndani ya miaka mitatu iliyopita zinatisha ambapo mwaka 2021 katika ajali 1,698, takriban watu 1,245 walipoteza maisha na wengine 2,023 walijeruhiwa. Mwaka 2022 katika ajali 1,720, takriban abiria 1,545 walipoteza maisha na zaidi ya 2,278 walijeruhiwa. Mwaka 2023 katika ajali 1,733, zaidi ya abiria 1,647 walipoteza maisha na wengine 2,716 kujeruhiwa na mwezi Januari hadi Juni mwaka 2024, kulikuwa na ajali 872 ambapo takribani abiria 816 walipoteza maisha na wengine 1,216 walijeruhiwa.

"Huu mfumo unakuruhusu kuingia kupitia linki ya https://pis.latra.go.tz na kisha utafahamu mwendokasi wa basi husika pamoja na vituo vya mabasi vilivyopo Tanzania Bara. Kwa upande wa mwendokasi, kama gari linaenda kwa mwendo hatarishi, unatakiwa kutoa taarifa haraka na endapo madereva na wamiliki wa mabasi wataona namna wananchi wanavyotumia mfumo



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Uchukuzi
Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini
Piga Bure : 0800110019/0800110020

**Mwendokasi wa Basi / Bus Speed**

Namba ya Gari (Vehicle Number): T440DCW
Muda wa Kuanza (Start DateTime): November 28th, 2024 13:00:24
Muda wa Mwisho (End DateTime): November 28th, 2024 14:00:24
Tafuta (Search)

**Mmiliki (Owner):** BUBELE LOGISTICS COMPANY LIMITED

| ID | Eneo (Location) | Muda wa GPS (GPS Time) | Mwendokasi wa Gari (Speed) |
|---|---|---|---|
| 1 | 24.19 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 14:00:23 | 78.98 |
| 2 | 22.05 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:58:14 | 83.99 |
| 3 | 20.91 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:57:23 | 79.99 |
| 4 | 19.23 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:56:05 | 79.99 |
| 5 | 17.02 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:54:23 | 77.98 |
| 6 | 16.88 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:54:17 | 76.97 |
| 7 | 13.10 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:51:20 | 67.00 |
| 8 | 9.98 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:48:22 | 79.99 |
| 9 | 6.30 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:45:22 | 81.97 |
| 10 | 6.08 KM W of Igunga Bus Terminal | 28/11/2024, 13:45:12 | 81.00 |

huu, watakuwa waoga na matokeo yake watapunguza mwendokasi na hatimaye tutapunguza ajali", amesema Mhe. Kihenzile

Vilevile anaeleza kuwa, PIS ni mfumo wa uwazi na rahisi kutumia na jambo zuri ni kwamba namba za LATRA za bila malipo zimewekwa katika mfumo huu, hivyo anawaasa wananchi endapo wataona gari walilopanda lina mwendokasi hatarishi au kuna uvunjifu wowote wa Sheria za usalama barabarani, wawapigie LATRA moja kwa moja kupitia namba zao bila malipo ambazo ni 0800110019 au 0800110020 na wao watashughulikia jambo lako kwa haraka.

Pia, anawaasa wamiliki wa mabasi kutumia mfumo wa PIS na amewataka madereva kuendesha mabasi kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za usalama barabarani ili kuepuka ajali na kufanya usafiri ardhini kuwa salama na wenye tija kwa wote.

Kwa upande wa wadau ambao ndio walengwa wa mfumo wa PIS, uwazi na urahisi wa kutumia mfumo huo. Bw. Abdul Wahid, ni mdau na anaeleza kuwa, "PIS inasaidia kuimarisha usalama wa safari za mabasi kwa kuwa sasa hivi naweza kuona mwendokasi wa basi nililopanda kupitia simu janja yangu wakati wowote mahali popote nitakapokuwa, endapo dereva ataendesha basi kwa mwendo hatarishi na mimi nitapaza sauti yangu kwa dereva na kondakta wake ili wapunguze mwendo na wakigoma nitawapigia simu LATRA kwa kuwa namba zao zipo kwenye mfumo."

Naye Bi. Elizabeth Mtemi, mdau wa usafiri anaeleza jinsi PIS inavyomtoa wasiwasi anapokuwa safarini. "Nikiwa safarini naweza kuangalia taarifa ya basi nililopanda kupitia PIS na nikafahamu ni muda gani nitafika mwisho wa safari yangu na mwendo kasi wa dereva ukoje. Vilevile kwa sasa naweza kumpokea mgeni wangu kwa urahisi na kwa wakati," amesema.

Mdau mwingine ni Bw. Enock Chilongola ambaye anashukuru kwa kupatiwa elimu ya PIS, "Elimu ya matumizi ya mfumo wa PIS imenisaidia kufahamu namna mfumo huu ulivyomrahisishia abiria kutambua taarifa ya basi linapoanza safari hadi mwisho wa safari na jinsi Mfumo huu ulivyo salama zaidi ukilinganisha na hapo zamani hakukuwa na taarifa hizi na ilikuwa si rahisi kwa mtu kujua ndugu yake aliyesafiri atafika muda gani."

CPA Habibu Juma Suluo ni Mkurugenzi Mkuu LATRA anaeleza kuwa PIS ni mfumo wa Kielektroni unaomuwezesha mtumiaji kupata taarifa za mabasi ya masafa marefu yanayotarajiwa kuwasili katika stendi iliyo karibu yake kwa lengo la kuondoa kadhia ya usumbufu au taharuki kwa abiria na wadau wa usafiri nchini na kuwezesha wadau kufahamu mwendokasi na mahala basi lilipo. Mfumo huu unapatikana kwa urahisi kwa anwani ya pis.latra.go.tz, na mwananchi anaweza kufungua mfumo huu kupitia simu janja au kompyuta.

Moja ya faida za kutumia mfumo wa PIS ni kwamba unarahisisha

upatikanaji wa taarifa muhimu za mabasi ya masafa marefu kama anavyoelezea CPA Suluo, "Mfumo huu unamuwezesha mwananchi kuwa na taarifa kwa ukaribu zaidi kuhusiana na mwenendo wa mabasi yanayowasili katika vituo mbalimbali nchini na kwa sasa kama una ndugu yako aliye safarini, huna haja ya kumpigia simu kufahamu alipo, bali utaingia kwenye mfumo, cha msingi ufahamu namba ya basi alilopanda. Vivyo hivyo kwa abiria akitumia mfumo huu wa PIS hatokuwa na haja ya kuuliza mahali alipo au muda anaotarajia kufika aendako."

Vilevile CPA Suluo anafafanua kuwa, mfumo wa PIS haupatikani tu kupitia simu janja ama kompyuta bali LATRA wamefanikiwa kufunga runinga kubwa katika kituo cha mabasi Magufuli kilichopo Dar es Salaam pamoja na kituo cha mabasi nanenane kilichopo Dodoma lengo ni kuongeza uwazi wa upatikanaji wa taarifa kwa abiria na wananchi wanaosubiri basi fulani liwasili katika vituo hivyo.

Naye Mhandisi Eliud Kataraihya, Mkuu wa kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) LATRA, anaeleza kuwa Mfumo wa PIS umetengenezwa kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri ardhini na kusogeza kwa karibu taarifa za kuwasili kwa mabasi katika vituo vya mabasi kwa abiria na wananchi kwa ujumla.

Vilevile anaongeza kuwa, akili mnemba imetumika kwenye mfumo huo na ndio imesaidia upatikanaji wa taarifa hizo kwenye vituo vya mabasi na mwananchi amepewa uwezo wa kuzipata taarifa hizo kwa njia rahisi na ya haraka popote alipo. Pia, mfumo unatoa taarifa kumi za mwisho zilizotumwa kupitia GPS na hivyo inarahisisha kufahamu muda wa kumpokea ndugu na hata kama atakuwa kaishiwa na chaji akiwa safarini utafika kwa wakati na kumpokea kwa kuwa taarifa zote unazo kiganjani kwako.

"Kwa sasa LATRA inakuletea taarifa karibu na wewe kupitia simu yako janja au kompyuta kwa kuingiza tu namba ya basi kwenye mfumo wa PIS na abiria akaweza kufahamu basi litawasili muda gani katika kituo alichopo na akaweza kusafiri kwa wakati uliopangwa bila kuchelewa pamoja na kufahamu taarifa ya mwendo kasi wa basi hilo kupitia taarifa kumi za mwisho za basi zinazosoma kwenye mfumo huo," anaeleza Mha. Kataraihya

Bw. Daudi Daudi ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), anasema mfumo wa PIS umeongeza thamani ya usafirishaji, "PIS umeongeza thamani ya usafirishaji kwani abiria aliyekuwepo safarini na yule anayetarajia kumpokea abiria huyo wanaweza kupanga muda wao vizuri hasa kwa yule anayempokea kwa sababu atakuwa na taarifa ya muda wa kuwasili kwa basi kituoni. Niwasihi watumiaji wote wa usafiri ardhini kuwa, waendelee kutumia mifumo ya TEHAMA ili iweze kuwaongezea thamani ya safari zao."


Mhe. Sophia Mwakagenda, Mbunge wa viti maalum Mbeya, ni mmoja kati ya viongozi walioipongeza LATRA kwa kutumia vizuri TEHAMA



katika utekelezaji wa majukumu yao kwa wananchi na hapa anasema, “Nitoe pongezi nyingi kwa LATRA kwa kuja na mfumo huu, nimejifunza vitu vingi hususan maendeleo ya kidigiti kwani naweza kutambua ndugu yangu yuko sehemu gani kwa kuangalia kupitia simu janja yangu na hakuna haja ya kufika stendi na kumsubiri mgeni wako kwa muda mrefu.”

Kwa upande wake, CP Awadhi Haji, Mkuu wa Operesheni na Mafunzo kutoka Jeshi la Polisi Tanzania, ameipongeza Mamlaka kwa ubunifu unaoendana na ukuaji wa teknolojia unaowezesha kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wanaotumia usafiri wa umma hususan mfumo wa PIS ambao umewarahisishia wananchi upatikanaji wa taarifa za safari za mabasi.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inaendelea kubuni mifumo mbalimbali itakayomsaidia watoa huduma, watumia huduma na itakayorahisisha kazi zake za kiudhibiti. Kwa hakika mfumo wa PIS ni mfano bora wa jinsi teknolojia inaweza kutumika kuboresha maisha ya kila siku ya wananchi na yeyote atakayebaini kuwa basi alilopanda lina mwendo hatarishi au kuna vitendo vinavyovunja Sheria, Kanuni na Taratibu za Usalama Barabarani, awasiliane na LATRA kwa namba bila malipo 0800110019/ 0800110020 au kwa mfumo wa e-mrejesho kupitia anwani ya https://emrejesho.gov.go.tz/ na suala hilo litafanyiwa kazi kwa wakati. Pia, mwananchi unapaswa kupaza sauti yako ili kuifanya sekta ya usafiri ardhini iendelee kuwa bora, salama na yenye manufaa kwa wananchi, wasafirishaji na Serikali kwa jumla.



**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini,**
**Makao Makuu S.L. P. 1742,**
**60 Mtaa wa Lusinde**
**41104 Tambukareli,**
**Dodoma.**